

Unawezaje Kujiieleza?

Kama ningekupigia simu mchana huu na ningekutaka ujielezee. Maelezo gani ungetoa? Labda ungetoa maelezo ya mwonekano wako wa nje. Labda ungetaka nijue kwamba una kimo cha urefu wa 6'0". Labda ungejieleza kwa kutumia ngozi yako, rangi ya ngozi yako, au pengine rangi ya nywele zako au uchache wa nywele?

Kuna namna yoyote ambayo ingekuwezesha kuelezea vipaji vyako? Labda ungesema una miguu myepesi kama kurungu au ungeeleza umashuhuri wako katika riadha au upungufu wa umashuhuri wa hilo.

Labda ungeeleza baadhi ya hurka zako kama vile unajaza fomu kwenye mtandao wa kutafuta wachumba. Mimi ni mcheshi, mchangamfu, mtu wa kutoka, maisha ya shamra shamra. Au ungejieleza kwamba wewe ni mkimya na unapenda kujituliza.

Kama ningekutaka ujieleze labda ungejieleza kwa shughuli unazozifurahia. Mathalani; napenda michezo, au napenda kusoma, napenda kushona, napenda kuona mapambazuko au machweo. Au napenda kuponi na kufanya manunuzi!

Navutiwa na kuona jinsi Yesu alivyojieleza katika injili nne. Hajawahi kutaja mwonekano wake wa nje, na uwezo wake wa riadha, matashi yake, au kwenye sherehe angecheza kwenye nafasi gani. Badala yake, anajieleza kwa namna ambayo inaonyesha kuwa Yeye ni mtumishi aliye tayari kutupa tunachohitaji.

Kwa hiyo, Hebu tumuulize Yesu, "Yesu unajielezeaje?" "Mimi ndimi mkate wa uzima," Yohana 6:48. "Mimi ndimi chakula cha uzima" Yohana 6:51. "Mimi ndimi nuru ya ulimwengu" Yohana 8:12. "Mimi ndimi mlango" Yohana 10:9. Mimi ndimi mchungaji mwema," Yohana 10:11. "Mimi ndimi mzabibu wa kweli," Yohana 15:1. "Mimi ndimi ufufuo," Yohana 11:12. "Mimi ndimi njia, kweli, na uzima," Yohana 14:6. Au labda "Mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo," Mathayo 11:29.

Jamani, tunajifunza jinsi Yesu alivyojitambulisha, ni dhahiri kuwa anajitambulisha kama mtu aliye kwa ajili yako. Kama mtu aliyepo kwa ajili ya ulimwengu. Kama mtu aliyepo kwa ajili kuturekebisha.

“Njoni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha. Jitieni nira yangu, mjifunze kwangu; kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu,” Mathayo 11:28-29

Hivyo safari nyingine mtu akikutaka ujitambulisha, pengine kabla hujajibu, tulia na kutafakari jinsi ambavyo alijitambulisha mara kwa mara, kisha endelea kutokea hapo.